



USAID
KUTOKA KWA WATU
WA MAREKANI



Wanafunzi wa Zanzibar wakisoma kitabu kwa pamoja.
Picha na: USAID

TANZANIA

TUSOME PAMOJA

Mradi wa Tusome Pamoja wa USAID unakusudia kuboresha mafunzo ya ujuzi wa stadi za msingi kwa madarasa ya chini ya elimu ya msingi, kuimarisha mifumo ya mafunzo ya ujuzi, na kuongeza ushiriki wa wazazi na jamii katika elimu. Mradi unafanya kazi katika mikoa mitano lengwa ili kuwafikia zaidi ya wanafunzi 706,724 katika darasa la kwanza hadi la nne, na pia walimu 26,000.

Licha ya maendeleo katika kuboresha usawa na upatikanaji wa elimu Tanzania, bado kuna changamoto kwenye stadi za msingi yaani kusoma, kuandika na kuhesabu kwa maelfu ya wanafunzi nchini. Kwa kuzingatia hali hii, USAID Tusome Pamoja ni mradi wa miaka 5 unaosaidia kuboresha kusoma, kuandika, na kuhesabu kwa madarasa ya chini ya elimu ya msingi. Kwa kufanya kazi na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi ya Zanzibar, na sekretarieti ya mkoa, Tusome Pamoja inafanya kazi kwa lengo la kuwafikia wanafunzi na walimu.

Mradi una malengo makuu matatu:

1. **Kuboresha Mafunzo ya Msingi kwa madarasa ya chini**, kwa kuboresha ufahamu katika masomo hayo na kutoa vifaa vya kujifunzia kwa wanafunzi wa elimu ya awali na darasa la kwanza hadi la nne. Tusome pamoja pia inakuza ufahamu na ujuzi wa walimu na viongozi wa shule kwenye masomo ya kusoma na kuhesabu, pamoja na kuanzisha vikundi vya kitaaluma vya walimu mashuleni.
2. **Kuimarisha Mifumo ya Elimu**, na hasa katika usimamizi wa watendaji wa sekta ya elimu, kwenye maeneo ya ushauri, ufuatiliaji, tathmini, na utafiti.
3. **Kuongeza Ushiriki wa Wazazi na Jamii katika masuala ya Elimu**, na hivyo kuimarisha ushiriki wao katika uongozi wa shule, usimamizi wa shule na elimu ya watoto wao.

MATOKEO

- Wanafunzi wa darasa la kwanza mpaka la nne katika mikoa ya mradi wa Tusome Pamoja wamepokea vifaa vipya vya kujifunzia; takribani vifaa milioni tatu vimesambazwa.
- Walimu wote wa darasa la kwanza ya 20,000) wamepata mafunzo kuhusu kufundisha kusoma na kuhesabu kwa madarasa ya chini, kuboresha maarifa na mbinu za kufundisha.
- Jumla wa wanajamii 6210 wamepata mafunzo ya kuhamasisha wazazi na jamii ili waweze kusaidia katika suala zima la elimu ya watoto wao.
- Tusome Pamojaitaendelea kuboresha mipango iliyopo kwenye kusoma, kuandika na kuhesabu ili kutafuta mbinu za gharama nafuu ambazo zinaweza kuendelezwa na kunufaisha nchi.

BAJETI Dola za Marekani milioni 67

MUDA

Januari 2016 – Januari 2021

MAENEO YA MRADI

- Zanzibar (Pemba na Unguja)
- Mtwara
- Morogoro
- Ruvuma
- Iringa

MTEKELEZAJI

RTI International

WASHIRIKA

Room to Read
Plan International
Miske Witt & Associates

MAWASILIANO YA USAID

Angela Cardenas
Mkurugenzi wa Ofisi ya Elimu
+255 746700 816
acardenas@usaid.gov

MAWASILIANO YA MTEKELEZAJI

Stephen Backman
Mkuu wa Mradi
+255 756 786 426
sbackman@rti.org

KWA TAARIFA ZAIDI

Tovuti: www.usaid.gov/tanzania
Facebook: USAIDTanzania
Twitter: @USAIDTanzania